# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

*Dar es Salaam*
*07 Agosti, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA
### RAIS SAMIA AZINDUA TUME KUCHUNGUZA WAHUSIKA WA GHASIA ZA UCHAGUZI 2025

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo tarehe 07 Agosti, 2026, amezindua Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Wahusika wa Ghasia na Ukiukwaji wa Sheria katika Matukio ya Ghasia za Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Tume hiyo, inayoongozwa na Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani Shaban Ally Lila, imepewa siku 150 kukamilisha uchunguzi na kuwasilisha ripoti pamoja na mapendekezo yake.

Rais Dkt. Samia amesema Tume imeundwa chini ya Sheria ya Tume za Uchunguzi (Sura ya 32), kufuatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Matukio ya Ghasia na Uvunjifu wa Amani Yaliyotokea Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025 iliyoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman.

Tume hiyo ya awali ilipendekeza kufanyika kwa uchunguzi wa kina ili kubaini wahusika wa matukio hayo na kuwezesha hatua muafaka za uwajibikaji kuchukuliwa.

Tume ina jumla ya wajumbe sita, akiwemo Mwenyekiti. Kati yao, Watanzania ni wanne, huku wajumbe wawili wakitokea nje ya nchi.

Wajumbe kutoka nje ni Naibu Jaji Mkuu wa Namibia, Petrus Tilainge Damaseb; na Jaji wa Mahakama ya Rufani Uganda, Barishaki Cheborion. Wajumbe wengine ni Majaji Wastaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Gad John Mjemmas, Awadh Mohamed Bawazir na Aishieli Nelson Sumari.



*Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano / ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania / ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

Rais Dkt. Samia pia amewataka Watanzania kutoa ushirikiano kwa Tume ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.



Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu